# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA RAIS IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### Mheshimiwa Spika

Awali ya yote nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na kutuwezesha kuhudhuria katika kikao hiki tukiwa katika hali ya amani na utulivu ambayo inatuwezesha kufanya shughuli zetu. Aidha, naomba kukupongeza wewe binafsi kwa namna unavyoliongoza Baraza hili kwa busara, hekima na umahiri mkubwa. Vile vile, nampongeza Naibu Spika, Wenyeviti, Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na Watendaji wa Baraza la Wawakilishi kwa kuendelea kushirikiana na Kamati na kutuongoza katika kutekeleza vyema majukumu yetu.

### Mheshimiwa Spika

Sisi Wajumbe wa Kamati hii kwa niaba ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi tunapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali

Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mafanikio yake ya uongozi kwa miaka mitatu. Kwa hakika hali ya amani na utulivu imekuwa ya juu hapa Zanzibar, ambayo imepelekea uchumi kuimarika, kuwepo ujenzi wa miundombinu, uimarishwaji wa sekta ya utalii pamoja na biashara. Sambamba na mshikamano wa hivi sasa ni mzuri sana kutokana na uongozi wake bora. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie uzima, busara na uwezo zaidi wa kuiongoza nchi yetu ili aweze kujenga misingi ya uchumi imara.

**Mheshimiwa Spika**

Katika kufanikisha majukumu ya kitaifa kwa ujumla, kamati yangu inaridhishwa na uongozi wa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla pamoja, Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kufanya kazi bega kwa bega na Mheshimiwa Rais katika kumsaidia na kumshauri kwenye masuala mbali mbali ya kuiletea maendeleo ya nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu na ujasiri wa kusimamia majukumu yao yenye lengo na nia madhubuti ya kuleta maendeleo endelevu hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**

Kipekee kabisa naomba kumpongeza Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kwa uteuzi wake wa nafasi hii mpya pamoja na umahiri wake unaomfanya kuongoza vyema ofisi hii. Napenda pia, kuwashukuru watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu mahiri Ndugu Saleh Juma Mussa pamoja na Afisa Mdhamini Pemba Ndugu Shuwekha Abdallah Omar kwa ushirikiano wao mkubwa na kamati wakati

wote wa ufuatiliaji wa shughuli za bajeti ya taasisi zilizo chini ya ofisi hii. bila ya kuwasahau watendaji wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia wakati wa kupitia Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mafungu yote yaliyo chini ya Afisi ya Rais Ikulu.

**Mheshimiwa Spika**

Kwa heshima kabisa napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Machano Othman Said — Mwenyekiti
2. Mhe. Maryam Thani Juma — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Zaina Abdallah Salum — Mjumbe
4. Mhe. Mussa Foum Mussa — Mjumbe
5. Mhe. Abdallah Abass Wadi — Mjumbe
6. Mhe. Haji Shaaban Waziri — Mjumbe
7. Mhe. Panya Ali Abdallah — Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman — Mjumbe
9. Ndg. Ali Alawy Ali — Katibu
10. Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir — Katibu
11. Ndg. Shawana Mohammed Haji — Katibu
12. Ndg. Amina Abeid Hemed — Mkalimani

**Mheshimiwa Spika**

Kwa kuwa jukumu la kamati kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa ajili ya mwaka mpya wa fedha, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeweza kuchambua na kujiridhisha vyema wakati ikipitia Mafungu ya Bajeti ya Ofisi hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 97(1) na 107(3) kwenye jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2020. Katika kutekeleza hilo, kamati ilikaa kujadili na hatimae kupitisha Makadirio kwa Afisi ya Rais Ikulu na leo hii kwa niaba ya kamati nawasilisha maoni yetu kuhusiana na bajeti iliyopo mezani.

**Mheshimiwa Spika**

Baada ya utangulizi huo, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa Afisi ya Rais Ikulu kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, ambapo Afisi inatekeleza shughuli zake kupitia Programu Kuu Tisa (09) na Programu Ndogo Kumi na Tano (15). Programu hizi zimejumuisha mafungu makuu manne, ambayo ni Fungu *A01* Ofisi ya Rais Ikulu, Fungu *A02* Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, Fungu *A09* Taasisi ya Afisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini, Fungu *A10* la Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu.

## FUNGU A01: OFISI YA RAIS IKULU

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia **Programu Kuu ya PA0102 "Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi",** kamati inatoa pongezi kwa idara hii kwa kuweza kuratibu warsha ya kitaifa ya kujenga uelewa kuhusu muongozo wa mpango wa biashara (Guided Trade Initiative GTI). Warsha hii ilijumuisha wadau mbali mbali wa Serikali na Sekta binafsi kutoka Zanzibar na Tanzania bara, ambapo lengo la uanzishwaji wake ni kwa ajili ya kurahisisha na kukuza biashara ili kufikia lengo la kuwa na soko kubwa Barani Afrika.

Kwa muktadha huu, kamati inashauri kuwa mambo yote yatakayojadiliwa katika warsha na mikutano kama hii na yenye tija kwa Zanzibar ni vyema tukayazingatia na kuyatumia katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Vile vile, kamati inashauri Zanzibar kushiriki kikamilifu katika mikutano ya kikanda na kimataifa kuanzia hatua za awali hadi kukamilika kwake kwani kupitia mikutano hii kunatengeneza fursa nyingi za ajira na kiuchumi kwa vijana wa nchi yetu. Sambamba na hilo, kamati inashauri Serikali kupitia programu hii kuzidisha kasi ya kutoa elimu kuhusiana na dhana ya Diaspora na umuhimu wa ushiriki wa wanadiaspora katika ajenda za maendeleo ya Zanzibar kwa kuwatumia Masheha wa Wilaya zote 11 za Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**

Katika kuunga mkono juhudi za Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Maapinduzi Mhe. Dkt. Husein Ali Mwinyi kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Rais Ikulu kuzidi kuwashajihisha wanadiaspora kusaidia katika utoaji wa huduma za kijamii pamoja na kuwekeza katika miradi mbali mbali ya kiuchumi hapa Zanzibar na Tanzania kwa Ujumla. Kupitia hotuba hii, kamati inatoa pongezi kwa Afisi ya Rais Ikulu kwa kufanikiwa kukamilisha kanuni za usajili wa wanadiaspora na ni wazi kuwa kanuni hizo zitawezesha mfumo wa usajili wa wanadiaspora wa Zanzibar kutambulika haraka na kiurahisi zaidi endapo utaweza kutumika kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**

Kupitia **Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu**, inayotokana na kifungu **PA0103** kamati imeridhika na hatua za uandaaji wa mkataba wa utoaji wa huduma kwa wateja ikiwa na lengo thabiti la kuboresha na kusimamia utoaji wa huduma hizo kwa njia inayozingatia viwango vya hali ya juu. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa **Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti,** kamati inatambua umuhimu wa utolewaji wa takwimu za kitaalamu katika maeneo husika kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa ambapo lengo kuu ni kuimarisha shughuli za mipango, kuandaa na kuchambua sera na kufanya tafiti. Hata hivyo, kamati inashauri tafiti zinazofanywa ziwe na tija kwa Serikali pamoja na maslahi mapana jamii ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**

Ofisi ya Rais Ikulu Pemba ina lengo la kuimarisha uwezo wa kiutendaji ikiwa ni pamoja na kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu Pemba. **Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu Pemba ya Kifungu PA0103**, Kamati inaishauri Ofisi kuendelea kuratibu na kufuatilia ahadi na maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa upande wa Pemba ili iwe njia rahisi ya kuungwa mkono na wananchi wakati akitafuta ridhaa ya kuiongoza Zanzibar kwa awamu nyengine. Aidha, Kamati inaipongeza Afisi ya Rais kwa kuendesha Kongamano la marekebisho ya Sera ya Mambo ya Nje lililofanyika kwa ushirikiano na Idara ya Ushirkiano wa Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi na Wizara ya Mambo ya Nje yenye lengo la kushirikisha wadau kutoka vyama vya siasa, NGOs, taasisi za dini, na makundi mengine ya jamii ili kujadili maboresho ya sera hii muhimu. Kamati inasisitiza kuendelezwa kwa ushirikiano huo hata baada ya sera kumalizika.

**Mheshimiwa Spika**

Vilevile, katika kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi, kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Mfumo mpya wa Sema na Rais Mwinyi (SNR) ambao una lengo la kuwapa fursa wananchi kuwasilisha changamoto au maoni yao kupitia taasisi za Serikali. Aidha, kamati imeridhika na mafanikio ya mfumo huu kutokana na hatua mbali mbali zinachukuliwa za kuhakikisha malengo yamefikiwa. Miongoni mwa hatua hizo ni kuweka utaratibu mzuri wa kuwasilisha malalamiko ya wananchi kwa masheha wa wilaya zote kumi na moja za Unguja na Pemba ambapo

mafunzo hayo yamesaidia kutoa mwanga kwa masheha juu ya Mfumo bora wa SNR katika kuwasilisha malalamiko.

**Mheshimiwa Spika**

Sambamba na hayo, kamati inaipongeza Idara hii kwa kutimiza miaka mitatu ya utendaji na mafanikio makubwa yamefikiwa na kufanya maadhimisho yenye kauli mbiu ya ***"SNR ni Daraja la Utatuzi wa Changamoto na Kero za Wananchi*"** ambapo kila muhusika anakadiriwa kupata taarifa kwa wakati. Hata hivyo, kamati imeona bado kuna changamoto kwa baadhi ya taasisi kutokutoa ushirikiano wa moja kwa moja na mfumo huu wa SNR na hivyo, kupelekea baadhi ya masuala ya wananchi kukosa ufumbuzi wa haraka. Kwa mantiki hiyo, kamati inashauri hatua kali za kinidhamu zilichukuliwe kwa watendaji au mhusika ambaye atakwenda kinyume au atakataa kutoa ushirikiano.

**FUNGU A02: AFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI**

**Mheshimiwa Spika**

Kufuatia hotuba ya Bajet ya Mheshimiwa waziri iliyosomwa, jumla ya TZS 3,107,600,000 zinahitajika kwa Afisi ya Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.  Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha hizo zinaingizwa kwa wakati uliopangwa, na malengo haya yanafikiwa kwa kusimamia na kuboresha uwajibikaji wa watumishi wa umma pamoja na kuhakikisha kila mtumishi anapata stahiki zake kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa kisheria.

**Mheshimiwa Spika**

Aidha, kupitia **Programu ya Usimamizi wa majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya BLM** na **Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Afisi ya BLM** Kamati inailipongeza Baraza la Mapinduzi kwa kutekeleza majukumu yake ya kutayarisha vikao Maalum vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake pamoja na kufanya uchambuzi wa Nyaraka na Taarifa kabla ya kuwasilishwa katika vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mapinduzi. Vilevile pongezi zaidi kwa taasisi hii kutokana na ongezeko la fedha za matumizi mengineyo OC, hii ni kutokana na matunda ya kazi nzuri wanazozifanya yenye lengo la kuhakikisha majukumu yao yanaleta ufanisi unaotakiwa.

**FUNGU A09: TAASISI YA AFISI YA RAIS UFUATILIAJI USIMAMIZI NA WA UTENDAJI SERIKALINI.**

**Mheshimiwa Spika**

Kama tunavyofahamu kuwa taasisi hii ina malengo makubwa juu ya usimamizi na uwajibikaji wa taasisi za umma hapa Zanzibar. Kupitia **Programu Kuu ya Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Serikali** yenye lengo kuu la kuharakisha utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ambayo inachangia katika mabadiliko ya uendeshaji na kutoa matokeo yenye ufanisi wa miradi ya kimkakati zanzibar. Kamati inatoa pongeza kwa taasisi hii kwa kufanikiwa kusimamia miradi ya kipaumbele ya ujenzi wa barabara na ukarabati wa miundombinu, miradi ambayo imekuwa ni chachu ya mabadiliko chanya kwa maendeleo ya Zanzibar.

Vile vile, kupitia taasisi hii ya *PDB* kamati inaendelea kutoa pongezi kwa idara hii juu ya uimarishwaji wa mawasiliano ikiwemo mfumo wa dashbodi ambao ulianzishwa kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa miradi ya kipaumbele inayotekelezwa kwa upamde wa Unguja na Pemba. Hata hivyo, kamati inashauri Serikali kuhakikisha wakandarasi wanaopewa miradi ya kimkakati wanaenda sambamba na mikataba ya miradi husika na kinyume chake hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mkandarasi huyo.

**Mheshimiwa Spika**

Kamati pia inashauri idara hii kuendelea kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo vya afya ili kufanya tathmini juu ya matumizi bora ya Mfuko wa Huduma za Afya (ZHSF) kwa Hospitali za Serikali na binafsi zinapatikana kwa wakati.

## FUNGU A10: TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU

**Mheshimiwa Spika**

Majukumu ya msingi ya Taasisi ni kutunza na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu kama urithi wa taifa. Vilevile kusimamia na kutoa miongozo juu ya namna bora ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka zote zinazozalishwa na kuhifadhiwa katika wizara, taasisi na mashirika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilizopo Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**

Kwa upande wa **Programu Kuu ya Utunzaji wa Nyaraka na Kumbukumbu kwa Matumizi ya Serikali na Umma** yenye lengo la kuwa na usimamizi imara, utunzaji nyaraka na kumbukumbu. Kamati imeelezwa kwamba taasisi hii imedhamiria kuhakikisha malengo yake yanafikiwa kwa kuendelea na harakati za ujenzi wa jengo jipya la ofisi lenye hadhi ya matumizi ya kitaifa na kimataifa, kamati imefarika kuona taasisi imefanikiwa kukamilisha mchakato wa kupata mkandarasi wa ujenzi wa jengo jipya la Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu lenye ghorofa tano (G+5) ambalo kumalizika kwake kutapelekea kutambulika zaidi katika ramani ya nchi bora zenye uhifadhi mzuri wa nyaraka na kumbukumbu za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kuingalia taasisi hii kama roho ya nchi katika kutunza na kuendeleza historia ya Zanzibar ili nyaraka na kumbukumbu zilizopo ziwe na mchango mkubwa katika sekta ya elimu na utamaduni wa nchi hii. Kupitia bajeti hii Kamati inaishauri Serikali kuzitatua changamoto zinazowakabili za upungufu wa vifaa vya kisasa ambavyo vinahitaji fedha nyingi na wataalamu katika kuendeleza uhifadhi wa nyaraka za muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,**

Halikadhalika, kamati inatoa pongezi za dhati kwa taasisi hii kwa kufanikiwa kuelemisha jamii kuhusu umuhimu na utunzaji na uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu yaliyofanyika kupitia maonesha ya Siku ya Chakula Duniani na Maonesho ya Kuazimisha Miaka 60 ya Sherehe za

Mpinduzi ya Zanzibar. Lengo likiwa ni kuwajengea uwezo watumishi na wananchi mbali mbali.
Kipekee, kamati inampongeza sa Mkurugenzi wa Idara ya Nyaraka na kumbukumbu kwa utendaji wake mzuri na weledi wa hali juu.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**

Kwa kumalizia hotuba hii, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa umakini na utulivu mkubwa. Ni wazi kuwa, Kamati yangu imeridhika na Makadirio ya fedha za Matumizi zilizotengwa kwa Ofisi ya Rais Ikulu na itaendelea kutoa msaada wa ushauri na mapendekezo yake katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Ni matumaini ya kamati kuona kwamba fedha zote zilizoombwa kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 zitatumika kama ambavyo imekusudiwa ikiwa ni pamoja na kusaidia kuweka ukaribu baina ya wananchi na Serikali yao.

**Mheshimiwa Spika**

Kwa ruhusa yako, sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili kumuwezesha Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu kufanikisha na kuweza kutekeleza yale waliyojipangia katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**

Kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuwasilisha na ***naunga mkono hoja.***

……………………………………..

**(Machano Othman Said)**

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**